

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Dar es Salaam
09 Novemba, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amemtumia salamu za rambirambi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) Mhe. Prof. Kitila Mkumbo kufuatia kifo cha aliyekuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Marehemu Lawrence Nyasebwa Mafuru.

Marehemu Mafuru amefariki leo tarehe 09 Novemba, 2024 katika Hospitali ya Apollo nchini India alipokuwa akipatiwa matibabu.

Rais Dkt. Samia anatoa pole kwa Watumishi wa Tume ya Mipango, ndugu, jamaa na marafiki kufuatia msiba huo.

Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu Mafuru mahala pema peponi, Amina.

A handwritten signature in blue ink.

Sharifa B. Nyanga
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu



Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi,
Jitokeze Kushiriki Uchaguzi